BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 12 Juni, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

48. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa ukanda wa Ngezi Vumawimbi umekuwa na mahoteli mengi ya kitalii ikiwemo Swahili Diver, Manter na Hyana. Na kwa kuwa suala la usafi wa mazingira ni muhimu sana katika maeneo yote, ikiwa ni pamoja na maeneo yanayozunguka mahoteli hayo.

(a) Je, Wizara yako ina mpango gani wa ukusanyaji wa taka zinazotoka katika mahoteli hayo.

(b) Kwa kuwa baadhi ya taka hizo ni hatari zikiwemo chupa na vigae, je, ni utaratibu upi unaotumika katika kuweka mazingira sahihi ya taka hizo.

(c) Je, ni lini Wizara yako itaanzisha kiwanda cha kusafisha taka ili kuongeza ajira na kuepuka usumbufu wanaoupata wamiliki wa mahoteli katika uhifadhi wa taka.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

119. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Hivi karibuni, Tanzania imekumbwa na changamoto za uhaba wa dola, hali ambayo inaathiri uchumi wa nchi. Uhaba huu wa dola unaweza kuwa na athari kubwa kwa biashara, uagizaji wa bidhaa, utalii na mifumo mengine ya kifedha nchini. Zanzibar ni moja ya eneo linaloathirika sana na uhaba huu wa dola.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka kushughulikia uhaba wa dola na kuhakikisha utulivu wa masoko ya fedha.

(b) Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuimarisha upatikanaji wa dola na kuzuia athari za uhaba huu kwa biashara na uchumi wa Zanzibar.

(c) Je, kuna mipango au sera za muda mrefu zilizowekwa ili kupunguza uhaba wa dola nchini.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

153. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Barabara ya Msituni/Msasani iliyomo ndani ya jimbo la Wingwi imo kwenye bajeti ya Serikali kwa ajili ya kujengwa kwa zaidi ya miaka miwili tofauti lakini hadi leo hii bado haijajengwa.

(a) Je, ni sababu zipi na za msingi zilizopelekea barabara hiyo kutojengwa hadi leo.

(b) Je, ni ipi kauli ya Serikali kwa wananchi hawa ambao kila siku wanatoa mali ghafi za ujenzi wa barabara.

262. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Hivi karibuni Meli ya ‘Flying Horse’ ilipata tatizo la mashine yake kuzimika katika nyakati mbili tofauti, kitendo kilichopelekea kufungashwa na chombo chengine na hatimae kurejeshwa bandarini. Hali hii pamoja na kufanikiwa kwake, ilizuwa hofu kubwa kwa wasafiri pamoja na familia zao.

(a) Je, ni makosa gani ya kiufundi (Technical errors) yaliyosababisha meli hiyo kuzima katika vipindi viwili tofauti.

(b) Kwa kuwa baadhi ya abiria waliathirika sana kisaikolojia na hivyo afya zao kuathirika, Je, ni kwa kiasi gani Serikali itawasaidia abiria hawa kuitaka Kampuni husika iweze kutoa fidia kutibu afya zao.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

159. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tatizo la upungufu wa mafuta limekuwa likiikumba sana Zanzibar katika vipindi tofauti tofauti jambo ambalo linapelekea kuwa usumbufu kwa wananchi na kushindwa kuendelea na shughuli zao za kila siku za kijamii na kadhalika.

(a) Je, ni changamoto gani zinazopelekea uwepo na upungufu huu.

(b) Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kuuangalia mfumo uliopo wa uingizaji wa mafuta na athari zake.

(c) Je, ni ipi kauli ya Serikali juu ya kuondokana na tatizo hili ambalo ni la aibu kwa Serikali.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

235. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

(a) Ni mashirika gani ya kimataifa ambayo yanawasaidia wabunifu wanaochipukia.

(b) Vipi na kwa namna gani Serikali inawasaidia wabunifu hawa katika kuwaunganisha, ili kuweza kunufaika na kile wanachokibuni.

(c) Je, Wizara yako haioni kwamba ipo haja ya kuwa na maonesho maalumu ya kazi za wabunifu tofauti na wajasiriamali waliozoeleka, ili kuipa msukumo tasnia hii ya ubunifu.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

71. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kwa kuwa dhamira ya Serikali ni kuendelea kuwakwamua wananchi kiuchumi, na tayari vifaranga aina ya mwatiko, kambare na sato vimeshaingizwa nchini.

(a) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuleta vifaranga vya aina ya changu, tasi na kolekole ili kuweza kuwasaidia wananchi ambao hawali sato, mwatiko na kambare.

(b) Ni lini Wizara yako itagawa vyombo vya mita nane na mita saba kwa wavuvi wetu walioko Pemba.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

274. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani): Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Katika kuwapunguzia ugumu wa maisha katika mfungo wa mwezi wa Ramadhani, Serikali ilikuwa na mpango uliokusudiwa kuleta akhueni ya bidhaa ikiwemo sukari kwa wananchi wa kawaida. Hata hivyo, mpango huo haukuwa wa mafanikio kwa kukosa kubuniwa na kuratibiwa mapema.

(a) Je, ni upi ufafanuzi wa Serikali kuhusiana na ununuzi wa sukari ya Mahonda kwa Shirika la ZSTC.

(b) Je, ni utaratibu upi ulitumika kwenye kodi ya ongezeko la thamani (VAT), katika msimu wa Ramadhani, wakati wa kuingiza bidhaa, wakati wa mauzo na Ukaguzi wa ZRA kwa wafanyabiashara wa sukari.

(c) Kwa vile msamaha wa VAT ulitolewa na Serikali wakati tayari sukari nyingi ilishaingia nchini na ilishalipiwa VAT, Je, ni upi utaratibu wa wafanyabiashara wa kurejeshewa malipo ya VAT ambayo tayari walishayafanya.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

45. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Kwa kuwa kuna baadhi ya 'scholarship' kwa vijana wanaomaliza darasa la 7 ambao wamepata ufaulu wa 'grade' A na B. Na kwa kuwa Wizara yako haitoi vyeti vya kumalizia masomo kwa daraja hili. Na kwa kuwa miongoni mwa masharti ya kupata 'scholarship' hizo ni pamoja na kuwa na cheti cha kumalizia skuli.

    (a) Vipi Wizara yako inatambua uwepo wa fursa hizi za 'scholarship'.

    (b) Je, Wizara yako ina utaratibu gani kwa vijana waliopata fursa za 'scholarship' nje ya nchi.

    (c) Je, Wizara ina idadi ya vijana wangapi wa daraja hili waliopata 'scholarship' na kuweza kusoma nje ya nchi.

109. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Hapo awali, Serikali yetu iliruhusu mfumo wa kujitolea kwa wafanyakazi, hususan walimu, katika shule zetu za Serikali ili kuongeza nguvu na ufaulu kwa vijana wetu. Pamoja na wazalendo wengi ambao walikubali kujitolea katika skuli zetu na kupewa ahadi ya kupewa kipaumbele katika ajira zitakapojitokeza, bado wengi wao wamesalia mitaani bila ya kunufaika na fursa hiyo.

    (a) Je, ni lini Serikali itawapa fursa ya ajira za kudumu walimu hawa waliojitolea kwa uzalendo mkubwa kwa nchi yao.

    (b) Je, ni ipi idadi ya uhitaji wa walimu kwa skuli za msingi, na ni hatua gani Serikali inachukua kuhakikisha mahitaji haya yanakidhiwa ili kuboresha elimu nchini.

**Wizara ya Afya:**

209. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    (a) Tathmini ikoje juu ya udhibiti endelevu wa maradhi ya mripuko hususan maradhi ya kipindupindu, hasa katika kipindi cha mvua.

(b) Tathmini ikoje juu ya punguzo au ongezeko la wagonjwa wa maradhi hayo ya mripuko kwa baadhi ya maeneo ikiwemo Magogoni na Darajabovu.

278. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Mgonjwa Asha Othman Ali kutoka Maziwani katika jimbo la Pandani awali alipelekwa na familia yake katika Hospitali ya Vitongoji ili kupata matibabu. Hata hivyo, baada ya kukosa tiba, familia yake ilimpeleka katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ili kupata matibabu bora. Baada ya kwenda na kurudi kwa takriban mwezi mzima kati ya Machi na Aprili 2024, akisubiri kufanyiwa 'Dialysis' ndipo alifanyiwa mnamo tarehe 04 Aprili, 2024 kwa kuchelewa sana na bila ya kutolewa maelezo yoyote. Hatimae mnamo tarehe 20 Aprili, 2024 mgonjwa huyo alifariki dunia.

(a) Je, ni ipi hali ya upatikanaji wa tiba kwa Unguja na Pemba kwa wagonjwa wanaosumbuliwa na matatizo ya figo.

(b) Je, ni sababu zipi zilizosababisha mgonjwa huyu kucheleweshwa kupata matibabu hadi akasababishiwa kifo.

(c) Je, ni utaratibu upi wa kufuatwa na malipo gani anastahiki mgonjwa wa maradhi ya figo kutoa ili kuweza kupata matibabu kwa wakati.

**Zanzibar,**
**12 Juni, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**